


Usalama kwanza

TARATIBU ZA HALI YA DHARURA



ZUIO LA KUTOKA NJE

Tishio liko ndani. Milango yote ya ndani na nje ifungwe. Hakuna anayeweza kuingia au kutoka kwenye jengo. Wanafunzi na wafanyakazi wote wajifiche. Taa na simu zote zizimwe.



SHIKILIA NA LINDA

Tishio liko nje. Wanafunzi na wafanyakazi wote wako ndani. Milango yote ya nje ifungwe. Hakuna anayeweza kuingia au kutoka kwenye jengo. Masomo yaendeleee ndani ya shule.



HAMISHA

Hali ya dharura. Jengo liondolewe watu kwa usalama na kimyakimya. Wanafunzi na wafanyakazi waende eneo la kukutanika nje ya shule. Vitu vyote binafsi viachwe, isipokuwa simu za kiganjani.

Taratibu hizi zinahusika kwa majengo na shule zote katika wilaya ya shule ya Francophone Sud.

Usalama Kwanza

Mawasiliano na wazazi katika hali ya dharura

- Kipaumbele cha shule ni kuhakikisha usalama wa wanafunzi na wafanyakazi. Wakati wa hali ya dharura, shule hazitajibu maombi yoyote ya taarifa na hazitatuma taarifa zozote kwa wazazi.
- Wilaya ya shule ya Francophone Sud itawasiliana na wazazi kupitia barua pepe, jumbe fupi, tovuti au vyombo vya habari mahalia.
- Tambua kwamba si maelezo yote yatakayoweza kutolewa ili kutohatarisha usalama wa watu wanaohusika au kuingilia mchakato wa uchunguzi unaofanyika.
- Baada ya tukio husika, taarifa zaidi zitashirikishwa na mchakato wa ufuatilaji utafanywa moja kwa moja kwa familia zinazohusika kupitia njia sahihi.

Je, taarifa zako za mawasiliano ni za hivi karibuni?

- Wazazi na walezi wanapokea jumbe za taarifa kupitia taarifa za mawasiliano zilizotolewa shulenii mwanzoni mwa mwaka wa shule kwenye fomu ya taarifa za mwanafunzi.
- Wazazi na walezi wanawajibika kuhakikisha taarifa za mawasiliano ni za hivi karibuni katika kipindi chote cha mwaka.
- Ikiwa taarifa zilizotolewa shulenii mwanzoni mwa mwaka wa shule zimebadilika katika mwaka husika, shule lazima itaarifiwe kwa sababu taarifa za mawasiliano za kwenye fomu ya mwanafunzi ndiyo zitatumika kuwasiliana na wazazi na walezi wakati wa dharura.

Taarifa:

<https://francophonesud.nbed.nb.ca/district-scolaire/protocole-d-urgence>



District scolaire
francophone Sud

Apprendre. Grandir. Devenir.